



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2016/2017

TOLEO LA WANANCHI



Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango
Kwa kushirikiana na Policy Forum



1. UTANGULIZI

Bajeti ya Mwananchi kama Mwongozo

Toleo la Bajeti ya Wananchi 2016/2017 kama ilivyokuwa kwa matoleo yaliyotangulia¹, linakusudia kutoa maelezo rahisi na wazi kuhusu **Bajeti ya Serikali** ya 2016/17. Kimsingi, Bajeti ya Serikali ni makadirio ya mapato na matumizi yanayoandaliwa na Serikali kwa mwaka. Ni chombo muhimu kinachotumiwa na Serikali kutekeleza maamuzi yake ya sera kwa vitendo kisiasa, kijamii na kiuchumi. Aidha, ni andiko ambalo linaonesha jinsi Serikali inavyopanga kukusanya mapato kupitia vyanzo mbalimbali na jinsi inavyotarajia kutumia kulingana na vipaumbele vilivyopangwa katika mwaka husika wa fedha.

Malengo ya Bajeti ya 2016/17

Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 imejikita katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi ananufaika na mgao wa rasilimali na matumizi yake. Bajeti inatilia mkazo umuhimu wa kutatua changamoto na matatizo yanayowakabili wananchi kwa ujumla, hasa wenye kipato cha chini. Msisitizo uko wazi kupitia kauli mbiu ya Mhe.Rais ya *‘Hapa Kazi tu’* yenye nia ya kubadili mwenendo wa watu waone kuwa ni vema kufanya kazi. Kaulimbiu ya bajeti ya 2016/17 ni **“Kuongeza Uzalishaji wa Viwandani ili Kupanua Fursa za Ajira”**

Katika kutekeleza bajeti ya 2016/17 Serikali ina malengo makuu ya kiuchumi mawili:

Kwanza, kukabiliana na changamoto zinazowakabili Watanzania ili kuleta matumaini mapya ya maisha mazuri zaidi kwa wananchi wetu, hasa wa kipato cha chini. Lengo hili litahusisha kufanya mageuzi makubwa katika utendaji wa Serikali hasa kurejesha nidhamu na uwajibikaji na kuondoa ufanyaji kazi kwa mazoea pamoja na kuimarisha uadilifu na usimamizi wa matumizi ya mali za umma na rasilimali za Taifa.

Pili, kujenga uchumi wa kipato cha kati kupitia utengemavu wa uchumi jumla na kuanzisha viwanda. Hali hii itawezesha kuongeza ajira hasa kwa vijana na kuongeza tija kwenye kilimo ili kuongeza kipato hasa kwa wale wenye kipato cha chini.

Serikali kupitia bajeti ya 2016/17 ina dhamira ya kweli na uamuzi wa kutekeleza miadi na ahadi zake kwa wananchi, ambazo zimeelezwa wazi kwenye:

- ☞ Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.
- ☞ Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21).
- ☞ Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (2015-2020).

¹ Tangu mwaka 2011/12



2. MWELEKEO NA MAKADIRIO YA UCHUMI JUMLA

Makadirio ya Malengo na shabaha za uchumi jumla katika muda wa kati ni kama ifuatavyo:

- ☞ Pato halisi la taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2016 kutoka 7.0 mwaka 2015.
- ☞ Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 5.0 mpaka 8.0 kwa mwaka 2016.
- ☞ Mapato ya ndani yakijumuisha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) yanakadiriwa kufikia asilimia 14.8 ya pato la taifa mwaka 2015/16 mpaka asilimia 16.9 mwaka 2016/17.
- ☞ Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia asilimia 13.8 ya pato la taifa mwaka 2016/17 kutoka 12.6 mwaka 2015/16.
- ☞ Matumizi ya Serikali kuongezeka kutoka asilimia 23.2 ya pato la taifa 2015/16 mpaka asilimia 27.0 mwaka 2016/17.
- ☞ Nakisi ya bajeti inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 ya pato la taifa mwaka 2016/17 kutoka asilimia 4.2 mwaka 2015/16.
- ☞ Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida inakadiriwa kuwa asilimia 7.9 ya pato la taifa mwaka 2015/16 na kupungua kufikia asilimia 7.5 kwa mwaka 2016/17.
- ☞ Akiba ya fedha za kigeni iweze kukidhi uagizaji wa bidhaa kutoka nje kwa kipindi cha kisichopungua miezi minne, ifikapo June 2017.

Mafanikio ya malengo na Shabaha za Uchumi Jumla kwa kiasi kikubwa yatategemea misingi ifuatayo:

- ☞ Kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na utengamano nchini, kikanda na duniani.
- ☞ Utulivu wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia.
- ☞ Kuwepo kwa hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi jirani.
- ☞ Kuendelea kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile pato la taifa, biashara ya nje, ujazi wa fedha, mapato, matumizi na huduma za jamii.
- ☞ Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia.
- ☞ Kuimarika kwa sera za fedha na za kibajeti zitakazosaidia kupungua kwa mfumuko wa bei na tofauti kati ya riba za amana na za mkopo.
- ☞ Kuzidisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi hasa uwekezaji katika viwanda.



3. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA SERIKALI 2016/17

Maeneo makuu ya vipaumbele vya Bajeti ya 2016/17

Kutokana na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 (unaotokana na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano) na pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, utekelezaji wa bajeti ya 2016/17 utalenga maeneo makuu ya vipaumbele yafuatayo:

- ☞ Shughuli za kuchochea ukuaji wa uchumi na uanzishwaji wa viwanda;
- ☞ Kutangamanisha maendeleo ya ki-uchumi na rasilimali watu;
- ☞ Mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji;
- ☞ Usimamizi na utekelezaji wa mpango.



Kero za wananchi zinazoshughulikiwa na Bajeti ya 2016/17

Bajeti ya 2016/17 inatarajia kushughulikia malalamiko ya wananchi kupitia hatua za kibajeti na kiutawala zitakazochukuliwa kama ifuatavyo:

- ☞ **Katika kuzuia na kupambana na rushwa katika utoaji wa huduma za umma**, Serikali imepanga kuanzisha mahakama ya mafisadi. Mbali na hilo, fedha zaidi zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha TAKUKURU na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuwezesha shughuli za usimamizi wa matumizi ya fedha na rasilimali za umma.
- ☞ **Hatua za kuzuia upotevu wa mapato** kwenye maeneo kama vile bandari, viwanja vya ndege na mipakani. Pia kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Kodi.
- ☞ Bila kuathiri ubora wa utoaji huduma, bajeti ya 2016/17 imeainisha wazi **hatua za kudhibiti matumizi** ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na yasiyo na tija kama kutumia kumbi za taasisi za Serikali katika kuendesha mikutano, semina na mafunzo; kupunguza sherehe za kitaifa zisizo za lazima; na kudhibiti matumizi ya simu, umeme na maji.
- ☞ Kuweka mkazo uongezaji wa thamani ya mazao na kukuza viwanda na biashara ili **kugeza na kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa mtazamo wa kibiashara**. Kadhalika, kupunguza ama kuondoa kabisa kodi zisizo na tija, zinazoathiri sekta na kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania.
- ☞ Serikali itaongeza juhudi **kutatua migogoro ya ardhi** kati ya wakulima na wafugaji, vijiji na hifadhi za taifa, wawekezaji na wakazi. Serikali pia itachukua hatua dhidi ya wale ambao wanashindwa kuendeleza mashamba na viwanja. Pamoja na mambo mengine, Serikali itaendelea na ununuzi wa vifaa vya upimaji wa ardhi, kuweka mipaka na fidia.


- ☞ Serikali itaendelea kushughulikia changamoto zinazotokana na **huduma zisizoridhisha za usafiri na usafirishaji**. Juhudi hizo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa barabara kufungua fursa za kiuchumi, ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*, ununuzi wa ndege mpya, meli za abiria ziwa Victoria na Tanganyika.
- ☞ Miradi kadhaa ya **umeme** itatekelezwa kama vile ya umeme vijijini na kukamilisha miradi inayoendelea mfano mitambo ya kufua umeme wa gesi ya Kinyerezi awamu ya kwanza na Kinyerezi awamu ya pili ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kuaminika kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani.
- ☞ Kuhakikisha **upatikanaji wa maji safi na salama** kwa ajili ya matumizi viwandani na majumbani. Pia, **upatikanaji wa huduma bora za afya** na **upatikanaji wa elimu bora**.
- ☞ **Mazingira wezeshi kwa sekta binafsi**, kwa kuboresha mazingira ya biashara ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwenye miundombinu kama vile barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, maji na nishati na uwezekano wa kuondoa ada, ushuru na kodi zisizo na tija ili kuvutia wawekezaji binafsi kuwekeza katika viwanda na sekta nyingine.
- ☞ **Uwezeshaji kiuchumi kwa makundi maalum kwa:**
 - ☆ Kutenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kupitia SACCOS;
 - ☆ Kutenga fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya makazi ya wazee na mahabusu za watoto, kununua chakula, dawa na mahitaji mengine ya watu walio katika mazingira hatarishi;
 - ☆ Kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ajili ya Wasanii, wabunifu, na wanamichezo;
 - ☆ Kufanya maboresho kadhaa kwenye maslahi ya wafanyakazi kwa kupunguza kiwango cha kodi ya mapato (PAYE) kutoka asilimia 11 hadi asilimia;
 - ☆ Kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha wachimbaji wadogo wa madini ili kuongeza tija na ufanisi;
 - ☆ Kujenga nyumba za makazi ya askari ili kukabiliana na uhaba wa makazi kwa askari nchini.

4. SERA NA HATUA MUHIMU ZA KUIWEZESHA BAJETI YA 2016/17

Sera na hatua muhimu za Mapato

Mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea na juhudi zake za kimkakati za ukusanyaji mapato ya kutosha hususan kwenye vyanzo vya ndani ili kuhakikisha utekelezaji wa bajeti. Mapato ya ndani ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 13,475.6 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 17,798 mwaka 2016/17 na hivyo kupunguza utegemezi wa bajeti. Hatua kadhaa za kisera na kiutawala zitachukuliwa kama ifuatavyo:

- ☞ Kutokomeza tabia na vitendo vyote (kama vile rushwa) vinavyosababisha upotevu wa mapato;
- ☞ Kuendelea kuimarisha usimamizi wa kodi katika maeneo yote ya ukusanyaji wa mapato (mfano bandari, vituo vya mipakani, viwanja vya ndege na maeneo ya uhifadhi makontena);
- ☞ Kuendelea kupanua wigo wa kodi na kurasimisha sekta zote zisizo rasmi;
- ☞ Kuimarisha uwezo wa taasisi za TMAA² na TEITI³ ili kuhakikisha kuwa kodi na mrabaha vinakusanywa zaidi kutoka rasilimali za madini;
- ☞ Kuimarisha ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato katika taasisi na mashirika yote ya Serikali;
- ☞ Kuongeza kasi ya matumizi ya mifumo na vifaa vya kielektroniki katika kukusanya mapato ikiwa ni pamoja na matumizi ya EFDs;
- ☞ Kuhakikisha matumizi ya hatua za uthaminishaji wa pamoja na ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa kuzingatia thamani ya majengo hayo katika Mikoa na halmashauri zote;
- ☞ Kufuta misamaha ya kodi iliyotolewa kwa maduka ya majeshi.



² TMAA ni kifupi cha Tanzania Minerals Audit Agency (yaani Wakala wa Ukaguzi wa Madini)

³ TEITI ni kifupi cha Tanzania Extractive Industries Transparency Initiatives (yaani Mpango wa Uhamasishaji uwazi katika Mapato ya Madini, Gesi Asili na Mafuta)

Maboresho ya Mfumo ya Kodi, Ada Tozo na Hatua nyingine za Mapato

Katika mwaka 2016/17, Serikali inakusudia kufanya maboresho kadhaa kwenye kodi mbalimbali, ili kuongeza mapato yakukidhi utekelezaji wa programu za kitaifa zilizopangwa na kupangiwa bajeti. Baadhi ya marekebisho muhimu ni kama ifuatavyo:

(a) Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148 imerekebishwa ili kuanzisha VAT kwenye:

- ☞ Huduma za utalii kama vile, kuongoza watalii, kuendesha watalii mbugani, utalii wa majini, kuangalia wanyama na ndege wa porini, kutembelea hifadhi na usafirishaji wa watalii ardhini;
- ☞ Huduma za kifedha isipokuwa riba kwenye mkopo.

(b) Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148 imerekebishwa ili kuondoa VAT kwenye:

- ☞ Maharage ya aina ya soya;
- ☞ Mbogamboga zote na mazao ya mifugo ambayo hayajasindikwa;
- ☞ Madawa ya kuchakata maji, vitamini na virutubishi;
- ☞ Bima ya vyombo vya usafiri wa anga ili kukuza sekta ya usafirishaji wa anga na hatimaye kukuza sekta ya utalii;

(c) Marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147, yanayopendekeza:

- ☞ Kuongeza ushuru wa bidhaa unaotozwa kwenye samani zinazotoka nje ya nchi kutoka asilimia 15 hadi 20 ili kukuza uzalishaji wa ndani wa samani kwa kutumia mbao zinazopatikana nchini;
- ☞ Kupiga marufuku utengenezaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene chini ya microns 50;
- ☞ Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye ada za simu katika kutuma na kupokea fedha badala ya ushuru huo kutozwa tu kwenye kutuma fedha.

(d) Marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 ili:

- ☞ Kuondoa msamaha ya kodi ya mapato kwenye malipo ya kiinua mgongo ya waheshimiwa wabunge ili kujenga usawa na haki katika utozaji wa kodi kwa watu wote;
- ☞ Kuondoa msamaha wa kodi kwenye mapato yote yatokanayo na hisa kwenye makampuni, hivyo kuongeza wigo wa kodi;
- ☞ Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato yanayotokana na ajira (PAYE) kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9;
- ☞ Kutoza kodi ya zuio kwenye malipo yanayofanywa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutokana na mapato ya uwekezaji ili kuendana na kanuni za Kodi zinazohusiana na haki na usawa;
- ☞ Kumpa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mamlaka ya kukadiria mapato yanayotokana na pango ili kutoza kodi ya zuio kwenye mapato hayo.

(e) Marekebisho ya sheria ya Elimu na mafunzo ya ufundi stadi, SURA 82 kwa kupunguza tozo ya kuendeleza ufundi stadi kutoka asilimia 5 hadi 4.5 kwa lengo la kuwapatia nafuu waajiri na kuhamasisha ulipaji wa tozo hii kwa hiari.

(f) Marekebisho ya sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki), SURA 124; ili:

- ☞ Kuongeza ada ya usajili wa magari kutoka Sh. 150,000 hadi Sh. 250,000 kwa magari na kutoka Sh. 45,000 hadi Sh. 95,000 kwa pikipiki;
- ☞ Kuongeza ada ya usajili wa namba binafsi za magari kutoka shilingi 5,000,000 hadi 10,000,000 kwa kila baada ya miaka mitatu kulingana na thamani halisi ya fedha.

(g) Marekebisho kwenye sheria zifuatazo; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, SURA 399; Sheria ya kodi ya Majengo ya Mamlaka ya Miji, SURA 289; Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290; Sheria ya Utawala wa Kodi ya mwaka 2015; na Sheria ya Rufani za Kodi, SURA 408, ili:

- ☞ Kuhamisha jukumu la kukusanya kodi ya majengo kutoka kwa ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Kwenda TRA;
- ☞ Kuwezesha TRA kufanya makadirio ya kodi za majengo na kuthaminisha majengo;
- ☞ Kuwezesha TRA kukusanya kodi ya majengo chini ya utaratibu wa sheria za kodi;
- ☞ Kuweka utaratibu mahsusi wa kupeleka mapato ya Kodi ya Majengo itakayokusanywa na TRA kwenda kwenye Halmashauri husika;
- ☞ Kuweka taratibu za kutatua migogoro itakayotokana na ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kwa kutumia sheria zilizopo zinazotumiwa na TRA;
- ☞ Kufanya mapitio ya misamaha ya Kodi ya Majengo ili kuhakikisha kuwa majengo mengi zaidi yanaingizwa katika mfumo wa utozaji kodi hiyo.

(h) Kufanya marekebisho kwenye sheria ya Msajili wa HAZINA (Mamlaka na Majukumu), SURA 370; ili:

- ☞ Kuzitaka wakala na mamlaka zote zilizo chini ya Msajili wa Hazina kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;
- ☞ Kukiondoa kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kutoka kwenye orodha ya taasisi za umma zinazochangia asilimia 15 ya mapato na badala yake kutakiwa kutoa gawio kwa Serikali kutokana na shughuli za biashara.

Sera za Matumizi

Katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu kwenye matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo. Aidha, hatua mbalimbali zitachukuliwa ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwenye matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na:


- ☞ Kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama vile maadhimisho ya kitaifa, posho za vikao, uchapishaji wa fulana, kofia, mifuko, vitabu vya kumbukumbu, kalenda, safari ya nje na mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi.
- ☞ Kutumia kumbi za taasisi za umma katika kuendesha mikutano, mafunzo na semina.
- ☞ Kutumia vyombo Serikali vinavyotoa huduma kama vile bima, usafirishaji barua, ufungaji wa mizigo, utoaji wa matangazo na usafirishaji.
- ☞ Kudhibiti matumizi ya magari ili kupunguza gharama za uendeshaji, matengenezo na ununuzi wa magari mapya.
- ☞ Kupunguza matumizi ya simu, umeme na maji kwa kuweka namba za siri, kutumia mita za umeme (LUKU) na kufunga mita za maji ili kudhibiti matumizi ya Serikali.
- ☞ Kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku Serikalini.
- ☞ Kuhakikisha kwamba mishahara inalipwa kwa wafanyakazi wanaostahili na ambao wapo katika vituo vya kazi.
- ☞ Kuunganisha Halmashauri zote nchini kwenye mfumo wa kielektoniki wa malipo.
- ☞ Kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa matumizi ya Serikali katika miradi ya maendeleo.

5. MAPATO: SERIKALI ITAPATA WAPI FEDHA YAKE?

Ili kuendesha shughuli zake na kutekeleza mipango na miradi yake kwa mwaka 2016/17, Serikali inategemea kukusanya **shilingi bilioni 29,539.6** kutoka kwenye vyanzo vifuatavyo:

- ☞ **Shilingi bilioni 15,105.1** zitatokana na kodi za mapato yanayotokana na ajira na mapato ya watu binafsi na kampuni (**kodi ya mapato**); Ununuzi wa bidhaa na huduma (**kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa**) na; Uagizaji na usafirishaji wa bidhaa nje (**ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa**).
- ☞ **Shilingi bilioni 3,358.4** zitazokana na mapato yasiyo ya kodi (ikiwemo faini, tozo, mauzo ya hati za zabuni na vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa).
- ☞ **Shilingi bilioni 3,600.8** kutokana na misaada na mikopo yenye masharti nafuu (ikiwemo misaada ya kibajeti, misaada na mikopo ya miradi na misaada na mikopo ya kisekta).
- ☞ **Shilingi 7, 475.3** kutokana na mikopo ya ndani na nje ya nchi (ikiwemo mikopo ya masharti ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi ambayo ni 1.5% ya Pato la Taifa).

Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2016/2017







6. MATUMIZI: NI KWA JINSI GANI SERIKALI INATARAJIA KUTUMIA MAPATO?

Matumizi yote ya Serikali kwa mwaka 2016/17 yanakadiriwa kufikia **shilingi bilioni 29,539.6**, ambayo yatumika kugharimia aina kuu mbili za matumizi:

- ☛ **Shilingi bilioni 17,719.1** zatumika kwenye **Matumizi ya Kawaida**. Fedha hizi ni kwa ajili ya kazi za kila siku za Serikali kama vile kulipa mishahara na ujira, pango la ofisi, mahitaji ya ofisi, gharama za usafiri, matengenezo madogo na ukarabati wa vifaa.
- ☛ **Shilingi bilioni 11,820.5** zatumika kwenye **Matumizi ya Maendeleo**. Matumizi hayo ni kwa ajili ya kugharamia miradi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, shule, hospitali, ujenzi wa mitambo ya maji na ununuzi wa mali.



Mgawo wa Bajeti kwa Mwaka 2016/2017



Matumizi ya Fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa


Katika mwaka 2016/17 jumla ya **shilingi bilioni 4,769.3** zimetengwa kama ruzuku inayopelekwa Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya). Kati ya hizo, **shilingi bilioni 3,925.9** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 843.5** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mgawo wa fedha zinazopelekwa Serikali za mitaa kissekta ni kama unavyoonekana hapa chini:

- ☆ Sekta ya Elimu Shilingi bilioni 2,958.
- ☆ Sekta ya Afya shilingi bilioni 719.7.
- ☆ Sekta ya Kilimo Shilingi bilioni 113.4.
- ☆ Sekta ya Barabara shilingi bilioni 50.96
- ☆ Sekta ya Maji shilingi bilioni 62.248.
- ☆ Utawala shilingi bilioni 864.94.

Mbali na kupelekwa fedha za ruzuku, **shilingi bilioni 665.4** zinazotarajiwa kukusanywa kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na zitatumiwa, ambapo **shilingi bilioni 266.2** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 399.2** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Matumizi kulingana na Majukumu ya Serikali

Matumizi yoyote (yawe ni ya kawaida au ya maendeleo), yamelenga katika utoaji wa huduma kulingana na majukumu ya Serikali kama inavyoonekana hapa chini.



Je Bajeti ya 2016/17 Itafanya kazi gani kwenye Sekta?

Matumizi kulingana na majukumu ya Serikali yamegawanywa kwenye sekta kadhaa ili kugharimia uendeshaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchi nzima. Mgao mkubwa (kama inavyoonekana katika chati hapo juu) ni kwenye shughuli zenye asili ya kiuchumi kama vile Viwanda, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Usafiri, Nishati na Madini.



Viwanda



Bajeti iliyotengwa kutekeleza majukumu ya sekta ya viwanda kwa mwaka 2016/17 ni **shilingi bilioni 81.9**. Aidha, Serikali itatumia **shilingi bilioni 50.9** kutekeleza mikakati ya "**Kuongeza Uzalishaji wa Viwandani ili Kupanua Fursa za Ajira**" kama vile: kufanya uthamini wa ardhi, mali na kulipia fidia maeneo ya uwekezaji; kufanya utafiti wa viwanda; kuendeleza miundombinu ya viwanda vidogo kupitia SIDO na; kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rahisi

na nafuu kwa ajili ya viwandani. Utekelezaji wa bajeti ya sekta ya viwanda utalenga hasa kukuza ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi. Kadhalika, ili

kuboresha mazingira kwa ajili ya maendeleo ya viwanda, fedha zimetengwa kwenye sekta nyingine kwa ajili ya kuboresha miundombinu inayohusu nguvu za umeme, maji, barabara, bandari na reli.

Dondoo za Matumizi mengine:

- ☆ **Shilingi bilioni 10** ni kwa ajili ya mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na mgodi wa chuma wa Liganga na zitatumika kwenye uthamini na uhamishaji wa wananchi;
- ☆ **Shilingi bilioni 9** ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya msingi ya viwanda eneo la viwanda la TAMCO, Kibaha;
- ☆ **Shilingi bilioni 6.1** ni kwa ajili ya kuwezesha SIDO kuboresha na kuanzisha maeneo ya viwanda vidogo Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Morogoro na Mtwara;
- ☆ **Shilingi bilioni 2.4** kuiongezea Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF) ili kuongeza wigo wa kutoa mikopo kwa viwanda vidogo;
- ☆ **Shilingi bilioni 1.7** ni kwa ajili ya Mradi wa Magadi Ziwa Natron/Engaruka ili kufanya upembuzi yakinifu, uthamini wa ardhi na kuwahamisha wananchi;
- ☆ **Shilingi bilioni 1** ni kwa ajili ya uanzishwaji wa miundombinu ya msingi kwenye eneo linalohusu kuongeza thamani ya ngozi katika mkoa wa Dodoma.



Kilimo, Mifugo na Uvuvi



Katika mwaka 2016/17, Serikali imepanga bajeti ya **Shilingi bilioni 1,560** kwa ajili ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kiasi kilichotengwa ni sawa na asilimia 4.9 ya bajeti yote, bila kujumuisha deni la taifa. Bajeti inalenga kuongeza uzalishaji, thamani na masoko ya mazao

yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi ili yaweze kutumika kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya uzalishaji na usindikaji. Serikali itahakikisha matumizi ya vifaa vya kisasa vya kilimo, mifugo na uvuvi, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na kuboresha miundombinu ya sekta kwa kujenga na kukarabati maghala na masailo (vihenge).

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 79.54** ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa masoko, maghala na masailo kwa ajili ya kuhifadhi nafaka, ununuzi na usambazaji wa vifaa vya hifadhi;
- ☆ **Shilingi bilioni 25.0** zitatumika kuwapatia wakulima wadogo ruzuku za pembejeo;
- ☆ **Shilingi bilioni 26.9** ni kwa ajili ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, vivile ununuzi na usagishaji wa mahindi kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko;
- ☆ **Shilingi bilioni 1.5** zitatumika kuendeleza uzalishaji kwenye sekta kwa kutoa mikopo kwa wakulima na wafugaji wadogo;
- ☆ **Shilingi bilioni 3.0** ni kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mashamba mapya ya uwekezaji na ajira kwa vijana;
- ☆ **Shilingi bilioni 21.7** ni kwa ajili ya kugharamia utafiti ili kuongeza tija kwenye uvuvi na mifugo;
- ☆ **Shilingi bilioni 18.2** zitatumika kujenga malambo; kujenga na kukarabati miundombinu ya uvuvi, minada ya ng'ombe na masoko; kuendeleza mashamba ya kuzalisha mitamba;

kutenga maeneo ya malisho; kutoa ruzuku kwa wavuvi na; kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari kubwa ya uvuvi;

- ☆ **Shilingi bilioni 5.9** kwa ajili ya kuendeleza ukuzaji wa viumbe majini kwa kuchimba mabwawa 5 ya samaki na kufunga mashine 5 za kuzalisha chakula cha samaki.



Usafirishaji



Sekta imetengewa **shilingi bilioni 5,470.3** sawa na asilimia 25.4 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la taifa. Kiasi cha bajeti kilichotengwa kwenye sekta ya usafirishaji mwaka 2016/17 kinatarajiwa kuimarisha maendeleo ya viwanda na rasilimali watu kwa kuboresha miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, hali ya hewa na mawasiliano.

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 1,347.7** ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara zitakazofungua fursa za kiuchumi;
- ☆ **Shilingi bilioni 1,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati ya kisasa kwa kiwango cha *standard gauge*;
- ☆ **Shilingi bilioni 161.4** zimetengwa katika Mfuko wa Reli kwa ajili ya ukarabati wa reli ya kati na ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa;
- ☆ **Shilingi bilioni 1,490** ni kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya tatu za abiria; ununuzi na ukarabati wa meli za abiria katika ziwa Victoria na Tanganyika; uboreshaji wa miundombinu ya bandari; na ukarabati wa viwanja vya ndege;
- ☆ **Shilingi bilioni 510** ni kwa ajili ya kuendeleza bandari zote.
- ☆ **Shilingi bilioni 832.3** kupitia Mfuko wa Barabara zitatumika kwa ajili ya upembuzi yakinifu na ujenzi wa barabara zenye jumla ya kilometa 3184 kwa kiwango cha lami, pamoja na madaraja 14 maeneo mbalimbali. Pia, kilometa 28 nyingine za barabara zitajengwa Dar es Salaam kupunguza msongamano wa magari.



Nishati na Madini



Katika mwaka 2016/17 Serikali imetenga kwenye bajeti **Shilingi bilioni 1,130**, sawa na asilimia 5.3 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la taifa. Lengo ni kuhakikisha kuwa nishati ya kuaminika inapatikana kwa ajili ya matumizi ya viwandani na majumbani.

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 587.6** zimetengwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini na kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini ili kuwezesha usambazaji wa umeme kwenye makao makuu ya wilaya na maeneo ya vijijini;
- ☆ **Shilingi bilioni 106** ni kwa ajili ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa jumla ya msongo wa KV 1020 ambazo ni Makambako-Songea, Dar es Salaam-Tanga-Arusha na Iringa-Singida-Shinyanga;

- ☆ **Shilingi bilioni 26.0** ni kwa ajili ya upanuzi wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji ya Rusumo na upanuzi wa gridi ya Kaskazini-Mashariki ya kusafisha umeme wa msongo wa KV 400;
- ☆ **Shilingi bilioni 229.2** kukamilisha mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi awamu ya kwanza na ujenzi wa mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi awamu ya pili;
- ☆ **Shilingi bilioni 15.6** ni kwa ajili ya kuiwezesha sekta ya nishati na madini na pia kuimarisha taasisi za sekta;
- ☆ **Shilingi bilioni 40.1** kusaidia maendeleo ya nishati mpya na nishati jadilishi;
- ☆ **Shilingi bilioni 5.0** kukamilisha upembuzi yakinifu wa mtandao ya usambazaji wa gesi katika mikoa ya Lindi na Mtwara Mikoa, pamoja na mradi wa bomba la gesi asilia;
- ☆ **Shilingi bilioni 10.7** ni kwa ajili ya maendeleo ya sekta ndogo ya Petroli ili kuharakisha utafutaji na upatikanaji wa mafuta ya petroli.



Elimu



Elimu ni njia muhimu ya kuifanya Serikali kufikia azma ya kuwezesha uchumi endelevu utaosaidiaia kufikia viwango vya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kupitia maendeleo ya viwanda. Kwa sababu, itawezesha nchi kuwa na jamii yenye ujuzi na ubunifu ambao ni muhimu kwa ajili ya sekta ya viwanda. Katika bajeti ya 2016/17, Serikali imetenga **shilingi bilioni 4,770** kwa ajili ya sekta ya elimu,

sawa na asilimia 22.1 ya bajeti ya Serikali bila kujumuisha deni la taifa. Bajeti ya sekta inalenga kwa kiasi kikubwa: Kutekeleza elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari nchi nzima; kutoa mikopo kwa wanafunzi elimu ya juu pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu nchi nzima; Kuinua ubora wa elimu na kujenga ujuzi wa kielimu unaotakiwa katika ngazi zote; Kuimarisha utafiti na matumizi ya sayansi na teknolojia kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi.



Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 3,069.5** zimetengwa kutekeleza mpango wa elimu bure;
- ☆ **Shilingi bilioni 44.61** ni kwa ajili ya mafunzo ya ufundi na Ufundi Stadi ambapo asilimia 81% zitatumika kusaidia vyuo vya Ufundi Stadi nchi nzima;
- ☆ **Shilingi bilioni 69.66** zitatumika katika maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwa kufanya ukarabati na kuendesha Vyuo Vikuu na Tume inayoshughulikia Sayansi na Teknolojia;
- ☆ **Shilingi bilioni 431.71** zitatumika kutoa mikopo kwa wanafunzi waliosajiliwa na taasisi za elimu ya juu;
- ☆ **Shilingi bilioni 43.75** zitatumika kuboresha elimu ikiwa ni pamoja na ukarabati wa vyuo vya walimu; kuimarisha ukaguzi; na uanzishwaji wa Tume ya Utumishi ya Walimu.



Afya



Katika mwaka 2016/17 **shilingi bilioni 1,988.2** zimetengwa kwa ajili ya sekta ya afya ambazo ni sawa na asilimia 9.2 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la taifa. Pamoja na mambo mengine, bajeti ya sekta ya afya inalenga kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wote.



Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 251.5** zimetengwa kupitia Bohari Kuu ya Madawa (MSD) kwa ajili ya ununuzi wa madawa, vifaa vya matibabu na vitendanishi nchi nzima; ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 71.0 ni kwa ajili ya madeni ya MSD;
- ☆ **Shilingi bilioni 646** ni kwa ajili ya huduma ya afya ya msingi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya;

- ☆ **Shilingi bilioni 10.1** ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na huduma za afya kwenye hospitali za taifa rufaa za kanda;
- ☆ **Shilingi bilioni 18.8** ni kwa ajili ya ukarabati na ukamilishaji wa ujenzi unaoendelea wa hospitali za mikoa nchini kote;
- ☆ **Shilingi bilioni 24.5** ni kwa ajili ya: uchunguzi wa kansa; mpango wa kupambana na kifua kikuu / ukoma; huduma ya magonjwa ya akili na matibabu ya kifua kikuu sugu;
- ☆ **Shilingi bilioni 20.0** ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matibabu kwenye Kituo cha matibabu ya Moyo cha Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na hospitali ya Rufaa ya Mbeya;
- ☆ **Shilingi bilioni 3.0** ni kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi nchini kote;
- ☆ **Shilingi bilioni 5.0** ni kwa ajili ya matibabu nje ya nchi watu watakaohitaji matibabu maalum yasiyopatikana nchini;
- ☆ **Shilingi bilioni 80.8** ni kwa ajili ya kuzuia maambukizi na matibabu ya VVU / UKIMWI.



Maji



Maji ni moja ya sekta zilizo chini ya jukumu la Serikali linalohusu **Makazi na Huduma za Jamii**. Kiasi kilichopangwa kwenye sekta ya maji kwa mwaka 2016/17 ni **Shilingi bilioni 1,020**, sawa na asilimia 4.8 ya bajeti yote bila kujumuisha deni la taifa. Malengo ya mwaka kwanye sekta ya maji ni: Kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini; kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji na usafi katika maeneo ya vijijini na mijini; Kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Bajeti ya sekta hasa ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwenye maeneo ya vijijini na mijini; kulipa madeni ya wakandarasi, na utekelezaji wa programu ya miradi ya Maji.

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 310.7** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa maji na usafi maeneo ya vijijini;
- ☆ **Shilingi bilioni 38.8** ni kwa ajili ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa;
- ☆ **Shilingi bilioni 63.4** ni kwa ajili ya miradi ya maji ya Same-Mwanga-Korogwe na Masai Nachingwea, pia usambazaji wa maji wa Ziwa Victoria- Shinyanga –Kahama;
- ☆ **Shilingi bilioni 102.6** ni kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji maeneo ya vijijini na mijini;
- ☆ **Shilingi bilioni 156.7** ni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa huduma za maji safi maeneo ya mijini;
- ☆ **Shilingi bilioni 152.3** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusambaza maji na usafi Dar es Salaam;
- ☆ **Shilingi bilioni 14.7** ni kwa ajili ya kusaidia usimamizi wa maji kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
- ☆ **Shilingi bilioni 54.6** ni kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa rasilimali za maji;
- ☆ **Shilingi bilioni 18.2** ni kwa ajili ya kujenga uwezo na kuimarisha taasisi za maji;
- ☆ **Shilingi bilioni 26.8** zimetengwa kupitia Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji;



Hifadhi ya Jamii



Mbali na juhudi za Serikali za kuboresha uchumi na sekta nyingine, uimarishaji wa hifadhi ya jamii ili kuboresha vipato na ustawi wa jamii umetiliwa maanani. Jumla ya **shilingi bilioni 387.9** zimetengwa kwa ajili ya masuala ya uhifadhi wa Jamii.

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 2.4** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwenye makazi ya wazee na mahabusu za watoto na; ununuzi wa chakula, dawa na mahitaji mengine ya watoto walio katika mazingira hatarishi;
- ☆ **Shilingi bilioni 59.0** zimetengwa kutekeleza mpango wa kila kijiji kupata Shilingi milioni 50 kwa awamu, ili kuwawezesha kiuchumi katika vikundi vidogovidogo vya kiuchumi;
- ☆ **Shilingi bilioni 15.0** ni kwa ajili ya kuwezesha Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini na Kuongeza Fursa za Ajira na Kazi zenye Staha. Programu itajumuisha: kukuza ujuzi kwa waajiriwa 13,400 katika sekta za kipaumbele ili kuendana na teknolojia; kutoa mafunzo kwa wanagenzi 4,600 kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo na waajiri; kuwezesha wahitimu 4000 kufanya mafunzo mahala pa kazi; kuimarisha vituo vya huduma za ajira ikiwa ni pamoja na mfumo wa taarifa za soko la ajira; kutoa mafunzo kwa watu 5,000; kutambua ujuzi kwa watu 5,000 unaopatikana nje ya mfumo rasmi;
- ☆ **Serikali imetenga asilimia 5.0** ya mapato ya ndani ya kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri) kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya vijana. Kadhalika, **Shilingi bilioni 1.0** zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mradi wa Maendeleo wa Vijana ili kuongeza uwezeshaji makundi ya kiuchumi ya vijana;
- ☆ **Shilingi bilioni 1.96** zimetengwa ili kuwezesha wanawake kiuchumi.



Demokrasia na Utawala Bora



Masuala ya Demokrasia na utawala bora ni kati ya majukumu muhimu ya Serikali yanayotekelezwa kupitia **Huduma za Jumla kwa Umma**. Katika mwaka 2016/17 **shilingi bilioni 81.9** zimetengwa kushughulikia masuala ya demokrasia na utawala bora.

Dondoo za Matumizi:

- ☆ **Shilingi bilioni 9.15** ni kwa ajili ya masuala ya katiba;
- ☆ **Shilingi bilioni 24.0** ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama na makazi ya Majaji;
- ☆ **Shilingi bilioni 3.55** ni kwa ajili ya shughuli za haki za binadamu na utawala bora;
- ☆ **Shilingi bilioni 1.68** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za kurekebisha sheria;
- ☆ **Shilingi bilioni 18.79** zimetengwa kwa ajili ya shughuli za vyama vya Siasa, ambapo Shilingi bilioni 17.20 ni ruzuku kwa ajili ya vyama vya siasa na shilingi milioni 230 ni kwa ajili ya Kituo cha Demokrasia Tanzania.

NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

- ⇒ Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- ⇒ Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020;
- ⇒ Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
- ⇒ Mkakati wa Taifa wa Madeni;
- ⇒ Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania;
- ⇒ Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati ya mwaka 2016/17;
- ⇒ Hotuba za Bajeti za Mawaziri 2016/17;
- ⇒ Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2016/17;
- ⇒ Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17;
- ⇒ Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016;
- ⇒ Sheria ya Matumizi ya mwaka 2016;
- ⇒ Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2016/17 (Juzuu Na. I –hadi IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea mitandao ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

.....(Kwa maoni zaidi kata ukurasa huu).....

Je, una mawazo gani, maswali, hisia (unafikiria nini), au una maoni gani kuhusu bajeti hii?

Je, unahitaji taarifa zaidi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki? NDIYO HAPANA

Kama ndiyo Je, unahitaji taarifa ya aina gani?

Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungehitaji sisi tukijue?

Je, kijitabu hiki kilikusaidia? ndiyo hapana kiasi Fulani

Je kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka? ndiyo hapana kiasi fulani

Tuma au fikisha sehemu hii

Wizara ya Fedha na Mipango,
Idara ya Bajeti ya Serikali,
1 Mtaa wa Madaraka
11468 Dar es Salaam
S.L.P. 9111, **DAR ES SALAAM**

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa: ps@mof.go.tz

Je, Utafanya nini na Taarifa hii?

Bajeti ya taifa ni taswira muhimu ya sura halisi ya kile ambacho Serikali inapanga kufanya kwa mwaka husika. Ukitaka kujua fedha yako ya kodi inakoenda, kama kuna mpango wa kuboresha elimu, afya, n.k katika eneo lako, unaweza kuangalia namna na jinsi ambavyo mgawanyo wa fedha unafanyika, hususan kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa muhtasari wa baadhi ya taarifa hizi kwa namna iliyo rahisi kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- ❖ Nyaraka zenye taarifa za bajeti ya Tanzania (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) na hasa, vitabu vinne vya bajeti ya taifa mbavyo vinapatikana katika Wizara ya Fedha (yaani Juzuu Na. I –hadi IV) .
- ❖ Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 9111, Dar es Salaam (tovuti <http://www.mof.go.tz>)
- ❖ Ofisi za Halmashauri na/au Maofisa katika eneo lako kama Mwenyekiti Mtendaji wa Kijiji au
- ❖ Policy Forum, S.L.P. 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na bajeti ya Taifa. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.